



COUNTY ASSEMBLY OF MOMBASA

OFFICIAL REPORT

Wednesday, 24th July, 2019
The House met at 10:20 a.m.

(The Speaker (Hon. Aharub Ebrahim Khatri) in the Chair)

PRAYERS

The Speaker (Hon. Khatri): Hon. Members you may be seated. Yes, Clerk?

MESSAGES

TRANSMISSION OF PUNGUZA MIZIGO, CONSTITUTIONAL AMENDMENT BILL, 2019

Hon. Members I have a Message which the title reads; *Transmission of Punguza Mizigo, Constitution Amendment Bill, 2019 to County Assembly...*

(Applause)

The letter dated 18th July, 2019 from Independent Election and Boundaries Commission (IEBC), Ref: IEBC/VREO/2/12/98;

1. *The Speaker, Mombasa County Assembly*
2. *The Speaker, Kwale County Assembly*
3. *The Speaker, Kilifi County Assembly*
4. *The Speaker, Tana River County Assembly*
5. *The Speaker, Lamu County Assembly*
6. *The Speaker, Taita County Assembly*
7. *The Speaker, Garissa County Assembly*
8. *The Speaker, Wajir County Assembly*
9. *The Speaker, Mandera County Assembly*
10. *The Speaker, Marsabet County Assembly*
11. *The Speaker, Isiolo County Assembly*
12. *The Speaker, Meru County Assembly*

13. *The Speaker, Tharaka-Nithi County Assembly*
14. *The Speaker, Embu County Assembly*
15. *The Speaker, Kitui County Assembly*
16. *The Speaker, Machakos County Assembly*
17. *The Speaker, Makueni County Assembly*
18. *The Speaker, Nyandarua County Assembly*
19. *The Speaker, Nyeri County Assembly*
20. *The Speaker, Kirinyaga County Assembly*
21. *The Speaker, Murang'a County Assembly*
22. *The Speaker, Kiambu County Assembly*
23. *The Speaker, Turkana County Assembly*
24. *The Speaker, West-Pokot County Assembly*
25. *The Speaker, Samburu County Assembly*
26. *The Speaker, Trans-Nzoia County Assembly*
27. *The Speaker, Uasin Gishu County Assembly*
28. *The Speaker, Elgeyo Marakwet County Assembly*
29. *The Speaker, Nandi County Assembly*
30. *The Speaker, Baringo County Assembly*
31. *The Speaker, Laikipia County Assembly*
32. *The Speaker, Nakuru County Assembly*
33. *The Speaker, Narok County Assembly*
34. *The Speaker, Kajiado County Assembly*
35. *The Speaker, Kericho County Assembly*
36. *The Speaker, Bomet County Assembly*
37. *The Speaker, Kakamega County Assembly*
38. *The Speaker, Vihiga County Assembly*
39. *The Speaker, Bungoma County Assembly*
40. *The Speaker, Busia County Assembly*
41. *The Speaker, Siaya County Assembly*
42. *The Speaker, Kisumu County Assembly*
43. *The Speaker, Homabay County Assembly*
44. *The Speaker, Migori County Assembly*
45. *The Speaker, Kisii County Assembly*
46. *The Speaker, Nyamira County Assembly*
47. *The Speaker, Nairobi County Assembly*

Hon. Members, again the letter title reference, *Transmission of Punguza Mizigo, Constitution Amendment Bill, 2019 to County Assemblies*, reference is made to the above matter. *The Independent Electoral and Boundaries; 'The Commission'* received a Draft Bill to amend the Constitution by popular initiative pursuant to Article (257) of the Constitution of Kenya, 2010 dubbed, *Punguza Mizigo Initiative*. The said initiative was promoted by *Third way Alliance Kenya*.

In compliance with Article (257) (4) of the Constitution of Kenya, 2010 the Commission undertook a verification exercise to confirm whether Punguza Mizigo Initiative was supported by at least one million registered voters. The Commission has since verified that the initiative has been supported by one million, two hundred and twenty-two thousand, five hundred and forty-one (1,222,541) registered voters. This is therefore to notify you that the initiative has met the required threshold as provided in Article (257) (4) of the Constitution of Kenya 2010.

Pursuant to Article (227) (5) of the Constitution of Kenya, 2010, the Commission hereby submit a copy of the draft Punguza Mizigo Constitution Amendment Bill, 2019 to your County Assembly for consideration within three months from the date hereof.

In conformity with Article 257(6) you are required to submit the decisions of your County Assembly to the Speakers of the National Assembly and the Senate.

Thank you Hon. Members. Yes, Clerk?

MOTIONS

SPONSORSHIP OF TEAMS PARTICIPATING IN FOOTBALL KENYA FEDERATION (FKF) LEAGUE

Yes Hon. Charles Kitula?

The Chief Whip (Hon. Kitula): Mr. Speaker Sir, I beg to move of the following Motion;

THAT AWARE that Part two (2) (4) (h) of the Fourth Schedule of the Constitution of the Republic of Kenya, 2010 mandates the County government to take charge of sports, cultural activities and facilities;

FURTHER AWARE that sports are a source of livelihood and one of the main contributors to our economy;

CONCERNED THAT many of our youths cannot achieve their dreams in sports especially football due to lack of support to football clubs from relevant Authorities;

NOTING THAT lack of support will continue affecting the growth of talents, economic reliability and as a result, many youths may engage in unlawful activities to make ends meet;

I urge this assembly to RESOLVE that:

The County government of Mombasa through the Department of Youth, Gender, Sports and Cultural Affairs to Partner with Constituency Development Fund (CDF) Committee, sponsors and other well-wishers to cater for participation fee, security fee, transport fee and wages for referees to all the Football Kenya Federation (FKF) registered teams in Mombasa County.

Mr. Speaker may I ask Hon. Moses Aaron to second the Motion.

(Hon. Aran seconded by bowing)

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Hon. Members. Hon. Members I now propose a question that the Motion by Hon. Charles Juma Kitula on, Sponsorship of teams Participating in Football Kenya Federation (FKF) League be considered in this House in the terms as moved.

(Question proposed and agreed to)

Yes Hon. Charles Kitula, you can now make your contribution.

The Chief Whip (Hon. Kitula): Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti na vile vile ningependa kutoa shukrani kwa Wabunge wenzangu kutoa ruhusa ili tuweze kujadiliana kuhusiana na Hoja ambayo nimeweza kuwakilisha katika Bunge letu tukufu siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti ama kweli sisi ni Wabunge ambao tumeweza kuchaguliwa kulingana na Katiba na vile vile tunawakilisha Wodi 30 na vile vile kuna Wabunge ambao waliweza kuteuliwa na Chama kulingana na masuala ambao wanaweza kutoa huduma katika Kaunti yetu ya Mombasa.

Vile vile Mheshimiwa Mwenyekiti katika Bunge hili kuna Mwakilishi wa vijana na vile vile katika Bunge hili kuna Kamati ya Michezo lakini kusema kweli kwa timu zetu katika Serikali ya Mombasa Kaunti imekuwa na wakati mgumu sana kuanzia hizi *tournaments* zinazoandaliwa na shirika la FKF huangaziwa kwamba gharama zote huwa wanaachiwa timu hizi kuweza kujigharamikia wenyewe binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti tukiangazia kwamba timu hizi hazina wafadhili ambao wanaweza gharamikia kuhakikisha kwamba timu hizi zinakabiliwa na changamoto na gharama ambazo zinakuja kila Jumamosi na Jumapili wanapokwenda katika michezo yao Mheshimiwa Mwenyekiti.

Jambo moja ambalo linawapatia changamoto zaidi ni masuala ya usafiri; ukiangalia Mheshimiwa Mwenyekiti timu hizi zetu za Mombasa Kaunti kila Jumamosi na Jumapili wanastahili kutoka katika eneo Bunge hili hadi eneo Bunge lengine kwa timu ambazo zina *participate* katika Kaunti yetu ya Mombasa na kuna timu ambazo zina *participate* katika *Division Two* na *Division One*. Mheshimiwa Mwenyekiti timu hizi zinastahili kusafiri katika Kaunti yetu hadi nje ya Kaunti zengine na vile vile hata katika *Province* nyingine.

Nikiangalia Mheshimiwa Mwenyekiti katika daraja la kwanza na la pili timu hizi inalazimika kuweza kuhakikisha katika kila mchuano kila Jumamosi na Jumapili lazima uweze kuweka ambulensi katika uwanja huo, ambulensi yameweza kugatuliwa masuala ya afya ambapo sisi kama Serikali ya Kaunti ya Mombasa ni jukumu letu kushughulikia masuala ya afya na mojawapo ni huduma za ambulensi lakini la kushangaza kwamba hawajawahi kupata ufadhili kutoka katika serikali yetu ya Mombasa kuwapatia angalau ambulensi. La musingi ni wao kugharamika kutoka kwa mifuko yao na ukiangalia ni wale wale wakufunzi, unapata ni meneja wa timu; unaweza pata ni *Coach* ambapo wengine hawana vibarua lakini wanalazimika kubisha hodi kwa Mheshimiwa, kubisha hodi kwako kama Spika, kubisha hodi kwa Mheshimiwa Hatimy, kubisha hodi kwa watu ambao wanafahamu mambo ya kandanda kuweza kusaidia timu hizi Mheshimiwa Mwenyekiti.

Jambo lengine ni upande wa usalama; Mheshimiwa Mwenyekiti kila Jumamosi na Jumapili timu hizi zinatakiwa kuweka askari wawili katika uwanja, askari wanachukua gharama chini ya zaidi shilling elfu tatu! Mheshimiwa Mwenyekiti kwa hio tukitaka inabidi unatoa *walk over*, ile timu inatoka katika Kaunti nyingine katika Kaunti yako kama hujaweka usalama basi mchezo hauendelei na wale waliokuja ambao ni wageni wanapata pointi za bure ama *walk over* kwa njia ya mtaani Mheshimiwa Mwenyekiti.

Vile vile *Referees*, masuala ya *Referees* kila timu inayocheza lazima iweze kugharimikia *Referees* Mheshimiwa Mwenyekiti; *Referees* katika kila wikendi ukiangalia timu hizi hawana kipato cha kuhakikisha kila wikendi wana pesa kuweza kugharamikia gharama hizi. Mheshimiwa Mwenyekiti, langu kuu ni kuweza kuhakikisha ya kwamba siku ya leo Wabunge wenzangu kwamba sisi ndio wawakilishi katika kata ndogo mbali mbali, hizi timu zinapokuwa na changamoto hutuwakilisha sisi katika mikutano ya Harambee kuweza kuwachangia ambayo mara kwa mara sisi kuna Harambee za matanga; kuna Harambee za kuchangia mgonjwa, tuna Harambee za masomo na sasa Harambee za michezo pia zimekuja, ilhali sisi watu wa serikali wa Kaunti za Mombasa ambayo ina uwezo wa kugharamikia gharama zote hizi, kuhakikisha kwamba timu zetu hazina shida.

Wabunge wenzangu ningependa siku ya leo muweze kuunga mkono Hoja yangu hii ambayo nimewakilisha katika Bunge hili maana timu zetu zinapata changamoto; timu hizi hazina wafadhili, timu hizi gharama zote zinakuja kwetu kama Waheshimiwa ambao ni wawakilishi wao lakini leo hii tukipeleka gharama hizi kwa Idara itakuwa rahisi kwa sababu wao wana bajeti na bajeti yetu ambayo mimi ni Mwanakamati wa Michezo katika maendeleo ya michezo Mheshimiwa Mwenyekiti tuliweka bajeti ya shilingi milioni 208 katika bajeti ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti sisi kama Kamati nikiingozwa na Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Samba tuliweza kuwaita wawakilishi wa hili shirika la FKF; kwanza tulianza na *Division* wa shirika la FKF South-Coast Branch wakatupatia bajeti yao. Mheshimiwa Mwenyekiti bajeti yao ya South-Coast Branch timu zote zinazo *participate* katika hio ligi bajeti yao ilikuja Ksh. 8,426,000 milioni. Vile vile katika FKF Mombasa Sub-Branch tulikuja nao na inaongozwa na Goshi aliweza kuleta bajeti yao katika Bunge hili na bajeti yao ilikuwa shilingi 4,734,000 milioni. Hizi ni gharama zote ambazo zinagharamikia katika timu zetu za mitaani kuanzia *Division Two* chini hadi juu Mheshimiwa Mwenyekiti.

Kwa hivyo Wabunge wenzangu leo nimesimama mahala hapa ya kwamba jambo moja liliweza kunitia huzuni kabisa, timu moja kutoka Likoni inaitwa Vibwangwa; Mheshimiwa Mwenyekiti Vibwangwa kuna siku timu iliweza kutoka katika Kaunti ya Kilifi, la kushangaza ni kwamba Kaunti ya Kilifi timu imekuja timu inatoa *walk over* ikiwa ni timu ya nyumbani.

Mheshimiwa Mwenyekiti hilo jambo lilinihuzunisha sana mimi kama mwanamchezo; kuangalia yoyote wewe kama *home team* unashindwa kugharamikia usalama na *Referee* lakini tuna serikali, tuna Waziri wa Vijana. Sasa wakati huu Mheshimiwa Mwenyekiti Gavana Joho ataweka sura yake wapi ikiwa timu kama Vibwangwa Likoni inatoa *walk over* na ana Waziri katika Idara kuhakikisha ya kwamba masuala ya michezo yanaangaziwa leo hii timu inatoa *walk over* ikiwa ni *home ground* mashabiki wamejaa pale kusubiri mchezo uanze mwisho wa siku unaambiwa kwamba *home team* imetoa *walk over*.

Wakati wageni kutoka Kilifi wamekuja kuweza kuwapa pointi za bure ni jambo la aibu, ni jambo la aibu kwetu kama wawakilishi wa Bunge la Mombasa na vile vile ni jambo la aibu kwa Gavana wetu pamoja na Idara yake ya michezo, kuangazia kwamba jambo kama hili limeweza kutendeka katika Kaunti yetu.

Kwa hivyo mimi Wabunge wenzangu leo nawakilisha Hoja hii na kwa mara ya kwanza tutafuatilia na Kamati kuhakikisha kwamba katika msimu unaokuja Mheshimiwa Mwenyekiti vijana wetu hawapati changamoto zozote, maana tayari tushaanza mwanzo kuanzia Jomvu, Likoni pamoja na Changamwe tumewapatia sare pamoja na mipira, linalofuata sasa ni kuhakikisha kwamba gharama hizi pia wanaweza kuwalipia kama Idara. Ahsante sana na ningependa Wabunge wenzangu waweze kuniunga mkono.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you very much Hon. Charles Kitula. Yes Hon. Mwaega?

Hon. Nyiro: Ahsante Mheshimiwa Spika hasa kwa kunitambua kwa jina la mzazi wangu Mwaega. Nataka mwanzo nimpongeze Mheshimiwa Kitula kwa kuleta Hoja hii muhimu, ama kweli Mheshimiwa Spika ukiangalia simu ya kila Mheshimiwa, kama hupati jumbe za nimefiliwa, niko na maiti mochari, niko na mgonjwa hautakosa ujumbe wa kwamba timu yetu Jumamosi inaenda *away game* na hatuna tikiti, hatuna pesa za *Referee!* Hizi ni jumbe ambazo tumezizowea na zimefanya Waheshimiwa wazidi kuwa wachochole ama maskini ilhali kama vile Mheshimiwa Kitula anavyosema tuko na bajeti ambayo tunaiielekeza katika Idara ya Michezo na Mheshimiwa Spika tukizungumzia mambo ya vijana na michezo, tunazungumzia swala ambalo limebeba vijana wengi na limepunguza sana ile hali ya ukorofi na utovu wa nidhamu katika mashinani.

Kwa hivyo ningependa kuunga mkono hii Hoja niseme kwamba huu mzigo sio mzito sana na itakuwa umepungua, si kupungua itakuwa ni majukumu yameenda mahali pake kwa sababu kama tuko na bajeti ya milioni 200 na unaona bajeti ambayo wakereketwa wa mchezo wa *football* wameleta bajeti ambayo ni kama milioni 12 itakuwa ni pesa kidogo sana tukiangalia kwamba tuko na bajeti ya michezo milioni 200 lakini ile fedha ambayo tunaitaka kusaidia vijana wetu ili waweze kufaulu katika wanayo azimia ni milioni tu 12 kwa mwaka mzima.

Kwa hivyo mimi naunga mkono niseme ya kwamba mambo haya yatiliwe mkazo na itakuwa vizuri ikiwa hatutapata yale maswala ya kwamba mambo haya yanahusu fedha, sijui mpaka yaende wapi, yarudi wapi, itakuwa si mambo mazuri. Vijana wasaidiwe na tukiangalia kwamba tukiazimia tunawasaidia kifedha na vile ambavyo pia naona Idara ile ya Michezo imeanza kuangalia vile viwanja vya mashinani kwa sababu ilikuwa ni masikitiko Mheshimiwa Spika kuona kuwa viwanja vinajengwa vya hali ya juu lakini ukienda mashinani ambapo talanta zimerundikana hakuna uwanja, tunajengea uwanja Kongowea, tuko na ule uwanja ambao uko kule Changamwe lakini ukienda mashinani kwingi viwanja watu wanacheza kwenye saruji wengine wanacheza kwenye hali ambazo ni mbaya.

Lakini nataka nipongeze Idara kwa sababu imeanza kulima vile viwanja na kuviweka katika hali nzuri; sasa ikiwa tutavilima vile viwanja na kuviweka katika hali nzuri lazima tujue kwamba tukivilima kuna vijana watakuwa wanatumia vile viwanja na wale vijana wakicheza tunataka wacheze ili wapande kwenda ngazi za juu. Kuna vijana ambao hivi sasa Mheshimiwa Spika kupitia kule kucheza vichochoroni wameweza kuonekana; wengine wamecheza Bandari nikipeana mfano mimi nina vijana wawili kutoka kwa Wodid yangu ambao wanachezea timu ya Bandari.

Na vile vile vijana wale wale saa nyengine wanaenda majaribio katika timu ya Harambee Stars lakini ukiangalia mahali walikotoka unashangaa walitoka kucheza wapi kwa sababu hakuna mtu amewaangalia mpaka wafike mahali ya kwamba wako Bandari ndio watu wawaone ah! kumbe huyu kijana ni wa Mombasa! Ni hali ya kusikitishana haya mambo tumeyaona kwa muda mrefu, kijana ametokea Likoni lakini tunafanya kushtuka kwamba ameitwa pengine kufanya majaribio Nairobi ndio tunashtuka kumbe ni kijana wa Mombasa lakini sisi wenyewe hatujui kwamba kuna kijana ambaye ana talanta ametambulika kwa sababu masuala haya yamewachwa. Vijana ni wengi, ukija Shanzu vijana ni wengi tena wanacheza kabumbu nzuri na mfano Mheshimiwa Spika unao; wewe mwenyewe uliweka ligi na vijana wa Shanzu wakanyanyua laki tatu kutoka kwako mfukoni, kumaanisha kwamba talanta ipo. Kwa hivyo mbona utowe laki tatu Mheshimiwa Spika na hapa kuna milioni mia mbili zimelala na hatujui zinafanya nini. Naunga mkono hii hali ili angalau hata wewe upumzike laki tatu twazingoja tena sisi Disemba, sasa ikiwa Idara haitahusika Mheshimiwa Spika tutaendelea kukufinya na hatutaki laki tatu Disemba hii twataka laki tano, sasa utajipanga. Naunga mkono na mzungu upungue kwa Waheshimiwa jamani, ahsante sana.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Hon. Mwaega. Yes Hon. Tobias Samba?

Hon. Samba: Thank you Hon. Speaker. I stand to support the Motion and let me first of all congratulate the Motion mover Hon. Charles Kitula; it has been a long journey that has been overdue. Hon. Speaker I also wish to take this opportunity to thank the Committee of Youth Gender, Sports and Cultural Affairs and today is a special day for me because it is my birthday, it is coming also with the birthday gift for the entire players of Mombasa County and also yesterday my predecessor wished me well and it was a good relief...

(Applause)

And I also wish to state in this Honourable House that each and every effort he made while he was the Chair we acknowledge and also we appreciate hoping and looking forward that we still work together and all the goodies that we are now discussing may be he is the founder when he was the Chair I was the Vice-Chair so we were working together so it is by good luck that it is now coming to effect.

Hon. Speaker I have got two issues; that is the reason why I support the Motion, number one in my Ward I have had several issues as far as the teams that are in my Ward are concerned, I had Spaki Young Stars, in fact they had to quit the tournaments because of lack of transport and security charges and we took this initiative so far we invited the tournament or rather league organizers that is FKF South Coast Branch and also Sub-Branch and whatever the Motion mover has stated that is what we agreed and also we had the goodwill of the Governor, in fact the Governor is the one who actually called the FKF South Coast Branch that they should not miss the invitation.

Hon. Speaker in my Ward in the just recently concluded AFCON; that number three, the left back number three comes from my Ward so I think you can see how Tudor Ward is blessed. Hon. Speaker we are going to make history in this House; as from today we will see most of the people will wish to join Football Clubs because it comes a time you play and there is nowhere you are going, may be transport that would enable you to access venues where the scouts that would have spotted you.

So Hon. Speaker this is the one of the best Motions that will go down in history that Mombasa County has adopted and if I look up there I can see the Chairman of one of the youth teams in my Ward who has been attacking me every now and then but for now at least he is here, he can see that we are planning every good for them and the goods that are coming will help and the issue of phone calls of here and now I think will stop, we will now be receiving phone calls of congratulations. Thank you Hon. Speaker, I beg to support.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Hon. Tobias Samba. Yes Hon. Athmani Salim?

Hon. Athmani Shebe: Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti kunipatia fursa hii kuweza kuchangia. Kwanza kabisa ningependa kutandika jamvi kwa kumpongeza Mheshimiwa Mwenza ambaye amekuja na Hoja hii.

Pili Mheshimiwa Mwenyekiti natia uhai Hoja hii ambayo imeletwa mbele na Mheshimiwa ambaye ni Kiranja wetu wa Bunge vile vile. Tatu Mheshimiwa Mwenyekiti imechelewa lakini imefika, Waheshimiwa wa leo changamoto ambazo tunapitia mashinani Mwenyezi Mungu ndiye anayejua zaidi katika maswala mazima ya michezo lakini tulitoka wapi, tuko wapi na tunaenda wapi? Safari imekuwa ndefu Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipitia misukosuko mikubwa sana na vile sasa pia tumefika tumeangazia baadhi ya changamoto nyingi ambazo zilikuwa zinakwaza vipawa vya vijana kule mashinani na nashukuru kumpongeza Mheshimiwa Mwenza wa Kamati ya Michezo kwa sababu tangu tulipomrithisha usukani wa kuongoza Kamati hii hatua kubwa imepigwa na mengi mazuri yanakuja, kongole na vile vile pia kumtakia siku yake njema ya kuzaliwa Mheshimiwa Mwenyekiti, *Happy birthday*.

Vile vile pia kongole kwa Mheshimiwa wetu wa kale Mwenyekiti ameonyesha ukomavu wa kisiasa namvulia kofia nikimueleza kuwa ameonyesha uongozi na huu ndio uongozi Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo kongole Mheshimiwa CV kwa kuonyesha uongozi. Mchezo ni nini, labda tujiulize Mheshimiwa Mwenyekiti, je, mchezo unalipa? Na ikiwa unalipa je unao uwezo wa kuondoa umasikini? Na ikiwa unao uwezo wa kuondoa umasikini, uchumi wetu kama taifa na kama Kaunti ya Mombasa utakuwa wapi? Mheshimiwa tukizingatia haya maswali niliyoyafululiza kwa mpigo kuwa jibu lake ni ajira zitapatikana kwa vijana kupitia michezo na vipaji vyao.

Kila mtu anajua Waheshimiwa Wenza changamoto tunazopitia mashinani, uchumi wetu umedorora kuwa kazi safari hii zimekuwa nadra kupatikana lakini tunawahamasisha vijana waweze kutumia vipaji vyao kuhakikisha kuwa wataweza kubuni ajira na wataweza kuzalisha rasilmali. Mimi ni mmoja wapo ambaye naamini falsafa ya kujajiri ndio utatengeneza mali, lakini ukiajiriwa maisha yako utabakia ukiajiriwa, kwa hivyo nashukuru Kaunti ya Mombasa na vile vile Waziri ambaye amekubali tushirikiane na yeye kuhakikisha kuwa tunawekeza zaidi katika vipaji.

Mimi nafikiri Waheshimiwa ambao wataweza kupinga Hoja hii basi kama si matahira sijui tutawaita namna gani Mheshimiwa Mwenyekiti kwa sababu kila mtu hii Hoja, kila mtu anajua uchungu na umuhimu wa hii Hoja, wewe ukiwa mfano umetuangazia na umetusaidia pakubwa mashinani lakini hatutaki kuwa maswala ya kuwa twaenda kutegemea mtu, hapana! Mheshimiwa ametanguliza kusema tumeweka takriban bajeti ya milioni 200 katika maswala mazima ya michezo, Jinsia na Utamaduni.

Kwa hivyo nampongeza Gavana amekuja kutambua kuwa kujajiri ndio kutazalisha rasilmali yetu ya Mombasa Kaunti; Waheshimiwa takriban bajeti ya milioni 200 si mchezo kwa hivyo ni wajibu wetu tuhakikishe kuwa hoja kama hizi zitakuwa zina mjadala mwingi sana Bungeni...

(Applause)

Ziweze kuungwa mkono ili natija ipatikane Mheshimiwa Mwenyekiti. Mimi leo nimeamka vizuri na naona nitalala vizuri kwa hii Hoja, kwa hivyo Waheshimiwa wenza tafadhalini ile mikakati ambayo Kamati ya Michezo inakuja nayo katika Bunge hili nafikiri natija zake mumeanza kuziona na hii ndio umuhimu Mheshimiwa wa Kamati za Bunge kuweza kuwajibika kuingia mashinani, kuangalia changamoto ni gani, suluhisho litapatikana namna gani, pesa hazifiki zitafanya vipi zifike mashinani Mheshimiwa Mwenyekiti.

Kwa hivyo nawaomba tuwe na imani kuwa wasaa ni ngwenje Mheshimiwa Mwenyekiti na safari hii ni punguza mzigo kweli...

(Applause)

Kwa sababu hapa Waheshimiwa tulikuwa tumelemewa, mimi sina mengi napenda tu kubananga wasaa niwapatie Waheshimiwa wenza kuzidisha uhai katika Hoja hii Mheshimiwa Mwenyekiti. Ahsante sana.

The Speaker (Hon. Khatri): Thank you Hon. Athmani. Yes Hon. Mgwisho Mwalimu?

Hon. Mwalimu Mgwisho: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Nachukua nafasi hii kwanza kumpongeza kinara wa Bunge hili kwa kuweza kuleta Hoja hii muhimu katika Jumba hili. Sisi viongozi sote ambao tuko hapa hakuna kiongozi ambaye hajafuatwa na timu hizi ili aweze kusaidia na pia nataka kuchukua nafasi hii kukushukuru Bwana Spika wakati ulipoanzisha *tournament* yako kule Uwanja wa Mbuzi, nafikiri wewe mwenyewe uliona vijana wanavyocheza kabumbu hasa wale waliotoka Likoni, timu yangu iliweza kutolewa katika *semi final* katika kinyanganyiro hichi cha Spika, timu yetu moja ya Likoni pia ikaingia *final*, ni kuonyesha kwamba vijana wa Likoni wako sawa sana upande huo wa michezo. Shida iliyoko ni kwamba, hawa Waheshimiwa wote nyuso zao ukiziangalia jua Hoja ishapita...

(Applause)

Wakati timu yetu ya Vimbwanga inapocheza *Wallahi* sisi viongozi huwa twapata shida sana, mimi mwenyewe nishawahi kuwasaidia Vimbwanga na kuna masharti mengi sana ambayo yamewekwa, ni lazima kuwa na usalama katika uwanja, kuwa na ambulensi katika uwanja, timu inayofuatia iweze kulipa kila kitu. Mimi mwenyewe nishawahi kuweka gari langu katika uwanja wa mpira kama ambulensi ili kusaidia atakayeumia. Hili ni janga kubwa sana, nakushukuru sana kinara wetu kwa kuleta Hoja hii, nina imani ya kwamba hizi milioni 200 ambazo zimetengwa kwa ajili ya michezo shida hizi ambazo tuko nazo zinazotukabili kama viongozi nafikiri zitakuwa zimepungua sana.

Narudi tena kukupongeza kinara wa Bunge hili kwa kuleta Hoja hii, mimi nasimama hapa kwa ajili ya kuunga mkono kwa dhati sana hii Hoja kwamba nini imani kwamba ishapita lakini twaizungumza kwamba ni Hoja lazima tuizungumze lakini kwa hayo machache Mheshimiwa Spika nasema ahsante sana...

(The Speaker (Hon. Khatri) exited the Chair)

(The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu) in the Chair)

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Yes Hon. Mwamwiri?

Hon. Athman Mwamwiri: Ahsante Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika awali ya yote nimtakie heri ya kuzaliwa Mwenyekiti wa Kamati ya Michezo, Jinsia na Tamaduni, *In shaa Allah* Mwenyezi Mungu ampe hekima na umri mrefu aweze kuwatumikia wananchi wake na hali kadhalika na wananchi wa Kaunti ya Mombasa.

Mheshimiwa Spika kwa mujibu wa muonekano wa ratiba ama jedwali la nne kwa Wang'eng'e wakasema *Fourth Schedule* (2) (4h), Mheshimiwa Mwenyekiti sehemu hii inapeana ama inagatua majukumu ya michezo kuwa chini ya serikali Gatuzi na tunaambiwa michezo utamaduni na shughuli za michezo na utamaduni tunaposema shughuli imejumlisha mengi yanayoshibika katika swala zima la michezo.

Mheshimiwa tukiangazia michezo katika Gatuzi letu la Mombasa tunajua ya kwamba ndio mchezo uliko kipao mbele na imekuwa utamaduni wa eneo hili miaka nenda miaka rudi Mheshimiwa na tutakubaliana kwamba soka au michezo ni maashilio, ni maponeo au posho kwa wale wengine wakasema tunaweza kupata riziki kutokana kwa michezo au vipaji hali kadhalika Wang'eng'e wakasema *livelihood*.

Hili halina mushkil Mheshimiwa Mwenyekiti, iwapo tutawekeza barabara katika swala zima la michezo na aghlabu katika swala la mchezo wa soka au kandanda tumeona jinsi ilivyo na inavyoweza kukidhi mahitaji ya changamoto ya swala la ajira katika Gatuzi letu na Kenya hii kwa jumla Mheshimiwa.

Mheshimiwa serikali yetu inaweza kwa sababu serikali jirani ya Gatuzi la Kwale zipo timu ambazo nazifahamu mbili zipo nyingi lakini nafahamu mbili; moja ikiwa ni AC Asad na moja ni Super Matuga ambazo sasa hivi wanacheza *nationwide* na wamekuwa wakigharamiwa shughuli zote, wanayo bajeti wametengewa kwa kila timu Kshs. 1.5Milioni kila mwaka.

Kwa kusimamia majukumu na shughuli za timu zile na kufikia sasa Mheshimiwa timu zile zimetupita kwa umbali katika Gatuzi la Mombasa kwa sababu katika ligi ile wanaweza kujitolea kwa sababu serikali Gatuzi inasimamia. Ni juzi tu Mheshimiwa AC Asad imeweza kucheza fainali dhidi ya Bandari ngao ya GoTv Shield na kuibuka nambari mbili katika mchakato ule kwa sababu wamewezeshwa kupitia kwa Serikali yetu.

Mheshimiwa sisi kama Gatuzi la Mombasa tunao uwezo kwa mipangilio kabambe kupitia kwa Kamati husika ambayo naipa kongole, ya kukubaliana kuafiki hili kuingia katika Jumba hili na kuweza kuipitisha Hoja hii iwe ni taratibu ilioko ya kudumu kwa serikali yetu kusimamia timu hizi si mwaka huu tuu, bali iwe ni swala la kuendelea tuweze kuziwezesha na kupeana fursa kwa vijana wetu kujitokeza na kuonekana na vipaji vyao huenda vikajalia kuwapatia riziki kupitia kwa hayo.

Mimi binafsi Mheshimiwa Mwenyekiti ni mlezi wa timu zinazoshiriki katika ligi hizi, takriban timu tano; kunao Soweto Rangers, iko katika Wodi yangu mlezi ni mimi, ninayo Zaragoza ipo katika Wodi yangu mlezi ni mimi, ninayo Change Youth ambayo tumeifanya kama *Academy* kunao vijana wa ngazi za ki umri tofauti, mlezi ni mimi. Hali kadhalika timu ya Vimbwanga ambayo Waheshimiwa wote wa Likoni tumekuwa walezi kwa timu hii, lakini uwanja wao wa nyumbani upo katika Wodi yangu.

Mheshimiwa imekuwa ni changamoto wakati mwengine timu zote tano zinacheza kwa siku moja kwa maeneo tofauti; hata kama ni ulezi lakini hapa ni kupasuka msamba Mheshimiwa. Mheshimiwa tumeona Idara ya michezo katika Gatuzi letu mwaka wa kifedha uliokamilika waliweza kufanyisha mazoezi ya mchezo wa *Golf* katika kila *Sub-County* ambalo Mheshimiwa natija yake hatujaiona, lakini swala lazima la michezo ya Kandanda najita yake ingekua bayana kwa kima kilichotengwa kwa lile zoezi Mheshimiwa Mwenyekiti.

Hali kadhalika Mheshimiwa Mwenyekiti sisi tulikuwa wenyeji wa zoezi la kuzawadia wachezaji waliobobea, almaarufu *Soya Awards*, zoezi lililofanyika ndani ya masaa sita na kima kilichotumika Mheshimiwa ni takribani Kshs. 10Milioni. Bajeti ya kusimamia timu zetu ni Kshs. 13Milioni kwa mwaka, kwa hili kuweka mbali suala la *Soya* tunao uwezo wa kukidhia timu zetu kwa mgao huu wa Kshs. 10Milioni kwa kuongezea tu Kshs. 3Milioni Mheshimiwa...

(Applause)

Kwa hayo Mheshimiwa binafsi nauunga mkono Hoja hii, na nina imani hakuna tahira katika Bunge hili kama alivyotangulia Mheshimiwa, japo kila mmoja ana hiari ya maoni na tunaheshimu maoni lakini suala hili ni la umuhimu kwa vizazi vyetu na sote kama Bunge nawahimiza tuweze kuliunga mkono. Ahsante Mheshimiwa.

(Applause)

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Yes Hon. Moses Aran?

Hon. Aran: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Kwanza ningependa kumpongeza rafiki yangu, ndugu yangu Kinara wa Bunge hili Mheshimiwa Kitula kwa kutuletea Hoja nzuri sana. Mheshimiwa Spika vile Mheshimiwa Shebe alisema aka *Mukono* hii Hoja si jambo la kutuweka hapa na umefika wakati kama tunaweza kuwa na tofauti za kisiasa ziwekwe kando na Kamati ya *Youth, Gender, Sports and Cultural Affairs* na mimi pia kama muakilishi wa vijana, *alias Youth Commander* 001 tuanze tutembe mpaka hii Hoja ifanyike Mheshimiwa Spika...

(Applause)

Nasikitika kwamba Hoja zapitishwa lakini hatuoni zaenda wapi? Lakini nataka kuhakikishia Bunge hili, na kwanza nampongeza Mheshimiwa Tobias Samba, MCA Tudor *Happy Birthday to you my brother...*

(Applause)

Na Kamati yako ambapo pia mimi ni Memba ningependa tafadhali tuhakikishe ya kwamba hii Hoja imetekelezwa; timu zinaumia Mheshimiwa Spika, alivyosema mimi na yeye twatoka eneo moja, tuko na Spaki Youth na Spaki Youngsters. Namuona Mwenyekiti wa Spaki Youth yuko hapa Mheshimiwa Spika; ninavyoongea leo saa 8:59a.m nimetuma tikiti, kila wiki ni lazima ung'anga'ne utume tikiti, inafika muda nikimuona Mwenyekiti naishi nae karibu, ni jirani yangu namuhepa kwa sababu nilimpatia ahadi ya kirongo nisingeweza, ananiambia tunaenda kucheza namwambia basi nitafanya. Akinikumbusha na mimi siku nikimuona inabidi nakata kona naingia kibandani ili apite Mheshimiwa Spika...

(Interruption)

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Hon. Member use a Parliamentary language.

Hon. Aran: Kata kona ni *sheng* Mheshimiwa Spika. Namuhepa, natoroka Mheshimiwa Spika siwezi kukutana naye kwa sababu nilimpatia ahadi ya kirongo; kwa hivyo naomba Waheshimiwa wote hapa hususan Waheshimiwa waliochaguliwa hawa wanapitia shida kila wiki ni lazima watume tikiti...

DISCLAIMER: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor Page*

(Applause)

Na wajua sisi ni binadamu, utapata leo Mheshimiwa Bwire ametoa tikiti, kesho nauli asipotoa zile timu hazitaki kuelewa, wanajua Mheshimiwa Bwire...

(Silence)

Mheshimiwa itabidi tupunguze mzigo na betri hapa. Unapata Mheshimiwa Bwire akitoa nauli leo, kesho akikosa zile timu hazitaki kuelewa wanatarajia ni lazima uwe nazo kila siku. Kwa hivyo mimi naomba tafadhali Mheshimiwa Spika tupitishe Hoja hii ipite ili timu zetu ziweze kupata huduma kutoka Mombasa Kaunti. Ahsante Mwenyezi Mungu awabariki.

(Applause)

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Hon. Members the Majority Leader is up.

The Leader of Majority (Hon. Mwidani): Ahsante sana Bwana Spika. Yangu ni machache; kwanza nampongeza Mheshimiwa kwa kuleta Hoja kama hii, na pia naipongeza Kamati ya *Youth, Gender and Sports*...

(Applause)

Bwana Spika huu ndio wakati watu watajua maana ya hili Bunge, wajua wengine wanaona tu labda ni pahali tunakuja kupita tu na kwenda...

(Applause)

Sisi katika kazi zetu moja ndio hii ya kutunga sheria. Kwa hivyo tukipitisha huu Mswada ni moja ya sheria, sasa isipotekelezwa ndio tutataka kujua mtu hatekelezi kwa sababu gani?

(Applause)

Mimi Bwana Spika nimefurahi sana kama mwakilishi wa Serikali ni kwamba tunamtia mtu *powers* za kufanya jambo, sasa akishindwa asije akatoa lawama, lakini hii ni sheria ambayo itampatia yeye nguvu kuweza kutumia hizo pesa bila kigegezi chochote, bila ya *Audit Report* na nini haina. Kwa sababu tayari sisi kama sheria tushapitisha pesa hii itengwe kwa sababu ya vijana. Bwana Spika kama kuna watu nafikiri waumia zaidi kwa hii mambo ya mipira na kutoa, hata mimi sasa ishafika pahali nimekwama kabisa.

Hata leo Bwana Spika sikudanganyi jana nimeuliza nataka kununulia vijana sare nikaambiwa itagharimu karibia Kshs. 25,000! Sikudanganyi Bwana Spika hali ni ngumu nashukuru nimezungumza na Mheshimiwa mwenzangu akanitafutia pahali nimepata za nafuu, kwa hivyo nitajaribu kununua hizo za nafuu lakini angalau vijana wangu waone wameng'ara. Kwa hivyo Bwana Spika mimi naiuunga mkono na *In Shaa Allah* Mwenyezi Mungu atatuwezesha vijana wetu waweze kuonekana vipawa vyao. Ahsante sana.

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Ok let Hon. Mohamed Hatimy then Hon. Renson Thoya to follow in that order.

Hon. Mohamed Hatimy: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mheshimiwa Spika mwanzo nachukua fursa hii kuunga mkono huu Mswada...

DISCLAIMER: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor Page 12*

(Applause)

Jambo la pili Mheshimiwa Spika twajua kuwa hii itakuwa ni nzito na hii stakabadhi ikienda kule kwa Idara iwe imekwenda ki sawa sawa. Kwa hivyo yangu ni kuomba mwenye hii Hoja abadilishe kusema kuwa *Constituency Development Fund* hakuna tena lakini aongeze *National Government Constituency Fund*, hakuna tena sasa CDF pekee yake kusudi hii stakabadhi ikienda iwe itakua ni stakabadhi safi.

Ya pili Mheshimiwa Spika nataka kuomba pia Kamati ya Michezo ikikaa kwa sababu kwa mujibu wa sheria hivi vitu vyote vimetajwa ni kusema kuwa kuna mambo ya Ambulensi na mambo ya usalama. Kisheria wewe ukikomboa ukumbi wa michezo inatakikana ule ukumbi wa michezo itoe vitu fulani nafikiri hata mukiangalia kwenye sheria za FIFA mutaona na CAF mutaona maneno haya.

Kwa hivyo itakuwa jambo la busara sio kuwa sisi tumepitisha sisi tulipe lakini ni lazima Kamati iweze kuwaita hawa FKF na wale wengine kwa sababu pesa ya serikali utaitumia leo na tunaona mambo vile yanavyokwenda ndani ya serikali yetu hivi leo angalia pale Hon. Rotich pale alipofikishwa. Tunataka tuwe tutafanya jambo ambalo litakuwa ni jambo la ki sawa sawa, kwa sababu hii inasaidia watoto wetu, hii inasaidia umma wetu wa Mombasa na jambo hili ikiwa litaweza kufanyika basi itakuwa ni jambo zuri sana Mheshimiwa Spika na mimi nashukuru kwa kunipatia nafasi hii nasema naunga mkono. *Thank you.*

(Applause)

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Yes I had ruled Hon. Thoya to follow.

Hon. Thoya: Ahsante sana Bwana Spika. Mimi nachukua nafasi hii kuweza kumpongeza Mheshimiwa Kitula kuweza kuja na Hoja hii; pia nampongeza ndugu yangu kwa siku yake ya kuzaliwa, tatu napongeza Bunge zima hili kwamba dalili zishaonekana ndani ya mwezi huu tumeweza kupitisha Miswada ambayo mengi ya hayo ni ya kukimu ama kuwekeza kwa vijana. Ni juzi tu kuna Mswada ambao tulikubaliana kwamba vijana wa mashinani waweze kupewa zile kazi za mikono ambazo zinatolewa na Kaunti; leo tunarudi kwa vijana kuhakikisha kwamba tunawawezesha vijana hao kusakata kabumbu ili iwe ni ajira kwao.

Mheshimiwa Spika ningependa kujulisha Bunge hili kwamba vijana ndio sehemu kubwa ya watu ambao wanaishi ndani ya Kenya hii, shida ni ajira; na ukosefu wa ajira athari yake ni kubwa zaidi. Mombasa hii imekumbwa na matatizo ya mihadarati, imekumbwa na matatizo ya usalama. Mimi ninaona kwamba tunajikomboa kutoka kwa shida hizi, na ni lazima tujikomboe kwa sababu vijana usipomalizana nao, watamalizana na wewe. Uamuzi tuko nao ndani ya Bunge hili, je tutamalizana na hao ama watatumaliza?

Mimi naona Bunge limekata kauli kwamba tunamalizana na hao, na imani yangu Mombasa hii itakuwa salama, itaweza kutoka katika lindi la mihadarati, utovu wa usalama na mambo mengi ambayo hayaridhishi. Mpira kama ilivyosemwa, kila mmoja amesema mimi nafikiri wikendi hii Jumapili nilitoa elfu tano, kuna timu ya HAKI Afrika ilikuwa inaenda na ni kila Mheshimiwa anasema lakini vile nimesema tunajikomboa hata sisi kidogo ile elfu tano tutaangalia upande mwengine. Kwa hivyo ninauunga mkono nikisema kwamba ni lazima tujikomboe na ni lazima vijana wetu tuwekeze kwao na kama hatutawekeza, tutakuwa na wakati wa kujilaumu sisi wenyewe. Naomba niunge mkono.

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Hon. Milka?

DISCLAIMER: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor Page*

Hon. Ngare: Thank you Mr. Speaker for finally giving me the opportunity to also give my sentiments. I think as you look around please be considering gender that they also need to be given a chance to voice their sentiments. I stand on a point of support for this very nice Motion brought about by our Chief Whip and I want to congratulate him for bringing the same to this Parliament in absentia even though he has left. I also want to congratulate the Chairman of Youth, Gender and Sports Mr. Samba and to wish him a happy birthday with many many blessings.

I will not repeat what has been said but let me just state that as state officers and as a County 001 it is our duty to help our youth to nurture their talent which finally may lead to some job opportunities so that they may also get a way of living, something to put on the table for themselves and probably their families.

So I do support the nurturing of talents through sports as the Chief Whip has clearly stated and also of utmost importance is that sports is a way of keeping healthy, physical fitness is very important for us and people who are physically fit are healthy, and a healthy nation is a wealthy nation. A Nation with people who are healthy is also a wealthy nation because we will be able to go out and carry out the activities; the youth will be able to be more productive as my colleague has clearly stated, that having these youths engage in sports will avoid the temptation of them sleeping into certain activities like engaging in drugs, engaging in robbery and such kind of things. They will be engaged in very productive activities as the English man says, "*An idle mind is a workshop of sin*", when we keep them busy they are going to be able to avoid things that may take them into certain temptations.

So I do support and when they travel, when the youths travel to other areas to go and engage in various sport activities they are exposed and they also meet other people from different cultural backgrounds and they learn new ideas, they learn new things and even can lead to mixed marriages to also help in things like tribalism we can avoid and create more unity in our country.

I therefore want to say that I support this Motion a 100 per cent; just as somebody has said, the Majority Leader has said that he was asked to contribute about Kshs.25,000 for a team that was in need of uniforms, there is a dance troupe at Kisauni which comes around where I live and my community. They approached me and they wanted uniforms because they are a cultural dance troupe, and when I went to inquire about the uniforms it was costing about Kshs.45,000, they are 15. So as a state officer, what would I have done? I have to sacrifice here and there, approach a few of my friends and I was able to buy them the uniforms, but this can be taken care of from our County budget through the Ministry of Youth, Sports and Gender so I support 100 per cent and I hope that all the other colleagues are in support of this Motion. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Yes Hon. Hamida, then Hon. Ibrahim.

(Hon. Omondi rose)

Hon. Omondi: Thank you.

(Interruption)

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Hon. Hamida?!

Hon. Noor: Thank you Hon. Member, I see somebody else is taking my name. I do support this Motion and I want to congratulate my fellow Member. I am a Member of the Youth, Gender, Culture and Sports and as the other Members have just said that this thing has to be supported fully, we want to engage our youth so that they can reach to the next level.

Let us go to the next level, let us see our children from Mombasa County going to other teams to play nationally so that we can be proud and say the Second Assembly from Mombasa County has done something better and we should congratulate ourselves with this Motion. I do urge my fellow Members please let us pass this Motion. Thank you.

(Applause)

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Yes Hon. Ibrahim?

Hon. Omondi: Thank you Mr. Speaker Sir and first of all Mr. Speaker I am very sorry for having just stood in for Hon. Hamida. This issue is very important Mr. Speaker Sir, It is really touching on me and that is why you saw the (??). Mr. Speaker Sir I just want to say this; this is one of the very important Motions we have ever come across in this particular Honourable House. Mr. Speaker Sir as you know that the residents of Mombasa County actually gave us the power to fulfill their dreams and also they gave us the wings to fly their message in this Honourable House; otherwise they would have a chance to come here all of them to speak but here we are speaking on their behalf. That was just to emphasize and I want to support fully this particular Motion with very credible reasons:

Mr. Speaker Sir, when the youths or when we engage our youths in this activity like for example soccer, you will agree with me that we are going to cut down the rate of crime in our surroundings and our environment because most of them will be engaged, that is number one.

When we engage our youths in this (??) activity we shall also try to control the issue of drug abuse Mr. Speaker Sir in our community which has cost our government a very big chunk of money to control it and therefore I give it a tick.

The talent search Mr. Speaker Sir, which is a very important characteristic; you will find that most of our youths who are engaged in football are not exposed to this higher level of activities and therefore they end up with or actually they do not know wherever they are but when we support them financially or when the County support them financially they will be exposed to the entire World and therefore you will agree with me that most of them will earn their living through sports, especially Soccer.

Mr. Speaker Sir I also want to say and to give a very good example which is well known to this House; when you look at people like who have come up or talented guys in soccer like Wanyama, look at people like Fabregas, look at people like Mariga, look at people like *Bomoa* these are people who have shown...

(Interruption)

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Yes Hon. Aran?

Hon. Aran: Point of Information Hon. Speaker! If I try to recall well Hon. Speaker Fabregas is not from this Country so Hon. Member is misleading this House, we should use the really examples like Aboud Omar from Spaki, Oliech, Hon. Kitula and me.

(Hon. Omondi off microphone)

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Use your microphone?

Hon. Omondi: Thank you. Mr. Speaker Sir let me base on things that are basic to support this particular Motion. Have i talked about the economic empowerment? I want also to give a very good example; I also have fallen a victim of being left behind and Mr. Speaker Sir I want to inform these Hon. Members that if I would be empowered from my youthful stage I could make a very good footballer in this particular Country and maybe I would not have just be in this House. You can see Mr. Speaker Sir what has happened but what happened is because I was not empowered economically, I was left to rot around and that is what these Hon. Members are saying that should not be repeated.

Mr. Speaker Sir I am finalizing my points; this is a gesture to devolution, It is a gesture to devolution because an essence of devolution is actually the resources to come down to the grassroots to come or flow down to the grassroots and if we empower youths in our Wards we shall also actually be giving a try to the devolution.

Mr. Speaker Sir this is a new dawn of leadership; leadership based on youth and women empowerment not wealth accumulation, leadership based on role modelling but not self-gratification. The time has come, the time has come Mr. Speaker Sir when the Members need to stand tall and speak loud so that this Motion must be passed and finally I want to warn those ones who had been sleeping on our Motions, those ones who have been killing these Motions; the people who are supposed to implement it and they do not implement Mr. Speaker Sir. I think this is going to be worse for them...

(Interruption)

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Your time is up!

(Applause)

Your time is up!

(Hon. Omondi still on the floor)

Hon. Ibrahim! Hon. Ibrahim your time is up! Yes Hon. Mohamed Omar Abrari?

Hon. Mohamed Abrari: Ahsante sana Mheshimiwa Spika. Mwanzo kabisa ningependa kumpa pongezi ndugu yangu Mheshimiwa Mwenzangu Kitula; zaidi mengi yashazungumzwa mazuri kulingana na Hoja hii lakini ningependa tu kutilia mkazo kwa sababu tumezungumza nyanja nzima ya michezo. Mimi kule kwangu ninakotoka Kongowea naona nimebahatika sana kuwa na nyanja nyingi za michezo, hivi tunavyozungumza hapa Kongowea kuna *National Boxing Tournament* ambayo inafanyika Kongowea nadhani hilo mnapasa kulijua na kusema kweli najivunia kuwa Mkongowea kwa sababu mwenye ameshikilia taji la *Feather-weight* ni Mkongowea taifa zima katika vijana na aliyekuwa mbeleni amesimamia taji hilo hilo ambaye anaitwa Modi Laiti alikuwa amesimamia taji hilo hilo la *Light weight*.

Tukienda mbele hivi majuzi nadhani Kongowea waliibuka washindi Mombasa nzima katika ligi ya *Neymar Junior* na wakatoka Kongowea kwenda kuwakilisha Mombasa nzima ama Pwani nzima kwa jumla Nairobi ili kwenda Brazil kwenye *Neymar Tournament*. Nadhani Mheshimiwa Spika utakubaliana na mimi tulikaa chini tukazungumza ni jinsi gani tutawasaidia vijana hawa kwenda kule na wengine wetu hapa nawashukuru mmoja akiwa ndugu yangu Mheshimiwa Nyundo na wengine waliingia mifukoni wakatoa pesa zao kuwa na mimi pamoja kwenda kuwasaidia. Vilevile tukienda katika nyanja nyengine ya michezo naona kuna nyanja baadhi nyengine tumeziwacha na ni muhimu sana tuzizungumzie; sisi watu wa Mombasa tumebarikiwa na bahari lakini nashangaa kipaji hiki cha kuogelea hatujakiangalia. Mimi kule ninakotoka nadhani mwajua wale vijana waliotoka kwenda kuwakilisha Kenya Africa Kusini ni vijana wanatoka Kongowea...

(Applause)

Na yule anayesimamia taji la Africa nzima sasa hivi Mr. Danford bado pia ni Mkongowea; kwa hivyo mimi kitu ambacho ningependa zaidi huu Mswada ni mzuri sana lakini naomba tungeutilia viungo kwa sababu si mpira pekee yake ambao tunafaa tuangaliee ambao ni kama ajira kwa watu. Nikiregelea bado Kongowea nafikiri mnajua kama kilabu kizuri cha *Skating* kinachowakilisha Kenya nzima *junior* chatoka Kongowea...

(Applause)

Kwa hivyo itakuwa uzuri sana katika Hoja hii tukiwa tutaongezea hii michezo mingine yote.

(Technical hitch)

Ahsante sana Mheshimiwa, naona kipaza sauti changu kimeleta mushkil. Mheshimiwa Spika mimi naunga mkono Hoja hii lakini naomba tuiongezee viungo kwa sababu kuna wenzetu wengine hawa wa *Basketball*, *Skating*, *Boxing* na *Swimming* naona ingekuwa vizuri Hoja hii ikawabeba wote kwa jumla wakaiweka kwa sababu yote ni michezo. Ahsante sana Mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Thank Hon. Mohamed Mohamed. I now call upon the mover of the Motion to respond.

The Chief Whip (Hon. Kitula): Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti na ningependa kuwashukuru Wabunge wenzangu kwa kuweza kuunga mkono na ningependa pia vilevile kuweza kuzingatia maneno ya Mheshimiwa Abrari kwamba hii Hoja ya leo ilikuwa inazingatia haswa zile timu za mchezo wa kandanda lakini sisi kama Kamati tunatayarisha sheria kuangazia michezo yote katika Kaunti yetu ya Mombasa. Kwa hivyo tutalitilia maanani na kama Kamati tutakuja na sheria ambayo itahusiana kabisa na timu zote ama michezo yote katika serikali yetu ya Mombasa.

Vilevile Mheshimiwa Mwenyekiti kuzingatia maoni ya Mheshimiwa wa Kamati ya Fedha kwamba ni hitilafu tu ya uchapishaji lakini kulingana na uamuzi wetu siku ya leo ningependa isome;

DISCLAIMER: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor Page*

The County Government of Mombasa through the Department of Youth, Gender, Sports and Cultural Affairs to partner with National Government Constituency Development Fund.

Mheshimiwa Mwenyekiti hii ilikuwa ni hitilafu ya uchapishaji tu imeweza tu kutokea lakini tunafahamishwa kuwa Makarani waliweza tu kusahau na itarekebishwa kama desturi yetu na Makarani wetu na utenda kazi wao. Kwa hivyo Mheshimiwa Mwenyekiti natoa shukrani na kuanzia sasa sisi kama Kamati tutahakikisha kwamba Hoja hii imeweza kutekelezwa kwa haraka wakati mitambo inapofunguliwa katika serikali yetu ya Kaunti ya Mombasa. Ahsante sana.

The Deputy Speaker (Hon. Mwalimu): Thank you Hon. Chief Whip. Hon. Members I now stand to put a question on the Motion on Sponsorship of teams participating in the football Kenya Federation League as read by Hon. Chief Whip, Charles Juma Kitula.

(Question put and agreed to).

(Applause)

Yes Clerk?

ADJOURNMENT

There being no other business the House stands adjourned until Wednesday 24th at 2:30p.m.

The House rose at 11:40 a.m.